

TANGAZO

1. **DAFTARI LA WANAHISA WA TANZANIA BREWERIES PLC**

Tunapenda kuwataarifu wanahisa wote wa Tanzania Breweries PLC (TBL) na umma kwa ujumla kuwa kuanzia tarehe 01 Agosti 2020 daftari la wanahisa wa TBL ikiwa ni pamoja na huduma ya ulipaji wa gawio vinasimamiwa na CSD & Registry Company Limited (CSDR) kampuni tanzu ya Soko la Hisa la Dar es Salaam.

2 **WANAHISA AMBAO HAWAJALIPWA GAWIO**

CSDR inawataarifu wanahisa wote wa makampuni tajwa hapo chini kuwa mpaka kufikia tarehe ya tangazo hili kuna idadi kubwa ya wanahisa ambao hawajachukua fedha zao za gawio. Hii inatokana na CSDR kutokuwa na taarifa zao za kibenki au namba za simu ambazo zitawezesha kulipa gawio:

- (i) **Vodacom (T) PLC**
- (ii) **TOL Gases Limited (TOL)**
- (iii) **TCCIA Investment PLC (TICL)**
- (iv) **Tanga Cement PLC (TCPLC)**
- (v) **National Investments PLC (NICOL)**
- (vi) **Mkombozi Commercial Bank PLC (MKCB)**
- (vii) **Dar es Salaam Stock Exchange PLC (DSE)**

Ili kuweza kulipwa gawio, mwanahisa anapaswa kututumia taarifa zake za kibenki (namba ya akaunti na jina la benki), namba ya simu ya mkononi pamoja na nakala ya Stakabadhi ya Umiliki wa Hisa (CDS Receipt) na kitambulisho (kimojawapo kati ya kitambulisho cha Taifa, Pasi ya Kusafiria, Leseni ya Udereva au Kadi mpya ya mpiga kura).

Mwanahisa anaweza kutuma taarifa zake kwa barua au kwa kujaza fomu ya kuboresha kumbukumbu za mwanahisa inayopatikana kwenye tovuti yetu **www.csdr.co.tz** na kutuma kwa anuani ifuatayo:

Msajili wa Hisa

CSD & Registry Company Limited
Kambarage House, Gorofa ya 2, Mtaa wa Ufukoni
S.L.P 70081
Dar es Salaam
Simu: 0746 160516 / 0677 070414
Barua Pepe: registrar@csdr.co.tz

Ofisi za CSDR ziko wazi siku za kazi Jumatatu mpaka Ijumaa saa 2 asubuhi mpaka saa 11 Jioni.